

16



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA**



**Kumb. Na.LD/MK/8544/ 34**  
Mkurugenzi Mtendaji  
Kituo cha Uwekezaji Tanzania  
S.L.P.838  
**Dar Es Salaam.**

**11/3/2024**

**YAH: KIWANJA NA.6 KITALU 'A' MBEZI/MWANZEGA [REDACTED], WILAYA  
YA MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu,  
Ninachukua fursa hii kuijulisha Ofisi yako kwamba, **kampuni ya Everwell Cable and Engineering Limited** imenunua maeneo kwa wananchi ndani ya Kijiji cha Mwanzega Kata ya Mbezi Wilaya ya Mkuranga kisha ikaandaa mpango wa matumizi ulioidhinishwa kwa Na.19/MKR/1189/2023. Kiwanja hiki kimepima na kusajiliwa kwa upimaji Na.189648 kikiwa na ukubwa wa mita za mraba **464,171** kwa matumizi ya **kiwanda**. Tunawasilisha taarifa hii kwako kwa ajili ya usajili wa Kampuni hii ili kupatiwa chetti ambacho kitaiwezesha Kampuni kuwasilisha maombi kamati ya ugawaji Ardhi Taifa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi **Na. 4 ya 1999, fungu la 20** sambamba na Sheria ya uwekezaji Tanzania **Na. 26 ya 1997**, kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) na kwa kuzingatia **fungu la 12 & 179 Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999** na Tangazo la Serikali **Na.72 la tarehe 4/5/2001**, Kanuni za Ardhi za 2001, **kanuni ya 9C (v)**.

Naambatanisha nyaraka za usajili wa kampuni, Mkataba wa kupata Ardhi, uthibitisho wa uraia wa wawekezaji, MoU and Articles of Association, na nyaraka zote muhimu kwa ajili ya mchakato wa usajili wa mwekezaji.  
Naomba kuwasilisha.

Chagile R.M  
K.n.y: Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Mkuranga.

**Nakala:Mkurugenzi Mtendaji (W).**

**Mkuranga** -Kwa taarifa  
Everwell Cable and Engineering Co. Limited  
**Dar es salaam** -Kwa taarifa na ufuatiliaji usajili TIC